# FANI KATIKA HADITHI FUPI

# ZA KISWAHILI

E. SANGAI MOHOCHI

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya: Master of Arts

Katika Idara ya Lugha na Isimu,

Chuo Kikuu Cha Egerton.

1995

## MUHTASARI

Tasnifu hii imejishughulisha na uhakiki wa fani katika hadithi fupi za Kiswahili ikiwa na lengo la kudhihirisha kuwa aina hii ya sanaa ni utanzu mahsusi wa fasihi wenye kaida mbalimbali zinazoongoza ujenzi wa fani yake na kuutofautisha na kazi nyingine. Utafiti huu ulichochewa na utambuzi kuwa hadithi fupi haijafanyiwa uhakiki kama kazi nyingine za fasihi. Aidha, katika fasihi ya Kiswahili kwa jumla, fani haijatafitiwa kama maudhui.

Swala la kimsingi katika tasnifu hii ni uchunguzi wa fani katika hadithi fupi. Japo hivyo, tumegusia kimuhtasari tu maudhui muhimu yanayowasilishwa na wasanii wa hadithi zilizohakikiwa kwani, kimsingi, fani na maudhui ni vipengele ambavyo hukamilishana. Ili kuyafanikisha malengo ya tasnifu hii, tumeteua hadithi nne kuwa msingi wa uhakiki huu. Hadithi zenyewe ni: "Siri ya Bwanyenye", "Wasubiri Kifo", "Kicheko cha Ushindi" na "Msiba wa Pamoja".

Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita. Sura ya kwanza ni utangulizi na imeeleza mada ya tasnifu, madhumuni ya utafiti, umuhimu wa mada hii, nadharia iliyotawala uchunguzi huu, upeo wake pamoja na yaliyoandikwa kuihusu mada hii. Sura ya pili ni muhtasari wa usuli na maendeleo ya hadithi fupi tangu enzi ya masimulizi hadi sasa. Tumechunguza pia athari ya ngano katika hadithi fupi andishi kifani na kimaudhui na, mwishoni mwa sura hii, tumejadili athari za jamii ya mwandishi katika utunzi wake wa kazi za sanaa.

Sura ya tatu imejikita katika dhana ya hadithi fupi. Hapa tumechunguza baadhi ya sababu zilizochangia kubaki nyuma kwa

hadithi fupi na kujaribu kulijadili swala tata la maana ya hadithi fupi. Aidha, tumeyahakiki maoni ya watafiti mbalimbali kuhusu hadithi fupi, dhima na umaarufu wake katika jamii, kabla ya kuhitimisha na baadhi ya mageuzi ama mabadiliko yanayoikumba hadithi fupi andishi.

Kiini cha tasnifu hii kinajitokeza wazi zaidi katika sura ya nne na ya tano kwani katika sura hizo tunahakiki vipengele mbalimbali vya fani vilivyoteuliwa kwa minajili ya utafiti huu. Sura ya nne inamulika kipengele cha lugha na, zaidi ya maelezo ya kijumla kuhusu lugha na fasihi, sura hii imehakiki matumizi ya kunga mbalimbali za lugha katika hadithi fupi za Kiswahili.

Katika sura ya tano wahusika wamechunguzwa kwa undani, kwanza katika fasihi kwa ujumla na, hatimaye, katika hadithi fupi. Tumeonyesha kuwa uumbaji na uwasilishaji wa wahusika katika hadithi fupi unatoa mchango usio haba katika kuitambulisha na kuitofautisha hadithi fupi. Wasanii wengi wanawaeleza wahusika wao na, kutokana na ufinyu wa mawanda, wahusika wengi hawakuzwi hatua kwa hatua na kuimarika vilivyo. Sura hii pia inachunguza ploti na usimulizi kama vipengele muhimu vya fani ya hadithi fupi. Hadithi fupi imedhihirisha kuwa na ploti sahili ambayo, aghalabu, huwa na msuko wa moja kwa moja na rahisi kufuatilia. Pili, inatumia mbinu mbalimbali za usimulizi lakini ile ya usimulizi maizi imejitokeza zaidi.

Katika sura ya sita ambayo ni hitimisho, tumetoa muhtasari wa kiini cha tasnifu nzima kwa kugusia, kimuhtasari, maswala yaliyoshughulikiwa kisha tukatoa hitimisho pamoja na mapendekezo yetu. Tumeeleza pia kwamba kuna vipengele kadhaa muhimu vya fani ambavyo hatukuweza kuvihakiki katika upeo wa tasnifu hii.

YALIYOMO


| | |
|---|---|
| MUHTASARI | i |
| SHUKRANI | iii |
| TABARUKU | vi |
| YALIYOMO | xv |
| **SURA YA KWANZA** | 1 |
| UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 MADA YA TASNIFU | 1 |
| 1.2 MAKISIO | 4 |
| 1.3 MADHUMUNI YA TASNIFU | 5 |
| 1.4 UMUHIMU WA MADA HII | 6 |
| 1.5 UPEO WA TASNIFU | 7 |
| 1.6 MISINGI YA NADHARIA | 11 |
| 2.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII | 16 |
| 3.0 NJIA ZA UTAFITI | 22 |
| **SURA YA PILI** | 23 |
| HISTORIA NA MAENDELEO YA HADITHI FUPI | 23 |
| 2.1 UTANGULIZI | 23 |
| 2.2 USULI NA MAENDELEO YA HADITHI FUPI | 23 |
| 2.2.1 HADITHI FUPI KATIKA MAANDISHI | 28 |
| 2.2.1.1 Miaka ya Kale | 28 |
| 2.2.1.2 Miaka ya Kati | 30 |
| 2.2.1.3 Karne ya Kumi na Tisa na Baadaye | 33 |
| 2.2.1.4 Nafasi ya Magazeti Katika Ukuzaji na Uendelezaji wa Hadithi Fupi | 37 |
| 2.2.1.5 Redio | 41 |
| 2.3 ATHARI YA NGANO KATIKA HADITHI ZA KUBUNI | 42 |
| 2.3.1 NGANO | 42 |
| 2.3.2 ATHARI ZENYEWE | 46 |
| 2.3.2.1 Athari Katika Maudhui | 49 |
| 2.3.2.2 Athari Katika Fani | 51 |
| 2.4 ATHARI YA MAZINGIRA YA MWANDISHI KATIKA HADITHI FUPI ZA KUBUNI | 57 |
| 2.4.1 SIASA | 60 |
| 2.4.2 UCHUMI | 64 |
| 2.4.3 UTAMADUNI | 68 |
| 2.4.4 DINI | 70 |
| 2.4.5 MAZINGIRA NA FANI | 71 |
| 2.5 KIMALIZIO | 75 |
| **SURA YA TATU** | 77 |
| DHANA YA HADITHI FUPI | 77 |
| 3.1 UTANGULIZI | 77 |
| 3.2 Utanzu Uliopuuzwa | 77 |
| 3.2.1 Sababu za Kupuuzwa | 81 |
| 3.2.1.1 Hadhira | 81 |
| 3.2.1.2 Mfumo wa Elimu | 82 |
| 3.2.1.3 Wahakiki | 83 |


EGERTON UNIVERSITY

3.2.1.4 Waandishi . . . . . . . . . . 84
3.2.1.5 Wachapishaji . . . . . . . . 85
3.3 Sifa za Hadithi Fupi . . . . . . . . . . 86
3.3.1 Mawanda . . . . . . . . . . . . . 86
3.3.2 Iktisadi ya Maneno . . . . . . . . . 88
3.3.3 Ufupi . . . . . . . . . . . . . . . 90
3.3.4 Ploti . . . . . . . . . . . . . . . 94
3.3.5 Wahusika . . . . . . . . . . . . . 96
3.4 Maana ya Hadithi Fupi . . . . . . . . . . . 100
3.5 Maoni ya Wataalamu Kuhusu Hadithi Fupi . . 103
3.5.1 Maoni Kuhusu Uandishi wa Hadithi Fupi . . . . . . . . . . . . . . . . 104
3.5.1.1 Ni Rahisi Kuandika Hadithi . 104
3.5.1.2 Ni Vigumu Kuandika Hadithi . 105
3.5.2 Maoni ya Kijumla . . . . . . . . . 107
3.6 Dhima na Umaarufu wa Hadithi Fupi . . . . . 109
3.7 Mabadiliko Katika Hadithi Fupi ya Kiswahili 111
3.7.1 Mabadiliko Katika Maudhui . . . 112
3.7.2 Mabadiliko Katika Fani . . . . . . 112
3.8 KIMALIZIO . . . . . . . . . . . . . . . . 115

**SURA YA NNE** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 117
LUGHA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 117
4.1 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . 117
4.2 Nafasi ya Lugha Katika Fasihi . . . . . . . 117
4.2.1 Majukumu ya Lugha Katika Fasihi . . 120

4.3 MATUMIZI YA LUGHA KATIKA HADITHI FUPI . . . . . . . . 123
4.3.1. Tamathali za Usemi . . . . . . . 123
4.3.1.1 Takriri . . . . . . . . . . 124
4.3.1.2 Sitiari . . . . . . . . . . 124
4.3.1.3 Tashbihi . . . . . . . . . . 125
4.3.1.4 Taswira . . . . . . . . . . 125
4.3.1.5 Chuku . . . . . . . . . . . 125
4.3.1.6 Tashihisi . . . . . . . . . 126
4.3.2 Methali na Misemo . . . . . . . . . 126
4.3.3 Kinyume . . . . . . . . . . . . . . 126
4.3.4 Muundo wa Sentensi . . . . . . . . 127
4.3.5 Nyimbo . . . . . . . . . . . . . . 127
4.3.6 Lugha ya Kishairi . . . . . . . . . 128
4.3.7 Tanakali Sauti . . . . . . . . . . 128
4.3.8 Nahau na Maneno ya Kiingereza . . . 128
4.4 WASUBIRI KIFO . . . . . . . . . . . . . . 129
4.4.1 Takriri . . . . . . . . . . . . . . 131
4.4.2 Sitiari . . . . . . . . . . . . . . 134
4.4.3 Tashbihi . . . . . . . . . . . . . 135
4.4.4 Taswira . . . . . . . . . . . . . . 136
4.4.5 Tashihisi . . . . . . . . . . . . . 137
4.4.6 Ishara . . . . . . . . . . . . . . 137
4.5 KICHEKO CHA USHINDI . . . . . . . . . . . 138
4.5.1 Takriri . . . . . . . . . . . . . . 140
4.5.2 Sitiari . . . . . . . . . . . . . . 140
4.5.3 Tashbihi na Tashihisi . . . . . . . 141
4.5.4 Taswira . . . . . . . . . . . . . . 142
4.5.5 Chuku . . . . . . . . . . . . . . . 143
4.5.6 Methali na Misemo . . . . . . . . 144

4.5.7 Kinyume . . . . . . . . . . . . . . . 145
4.5.8 Tanakali Sauti . . . . . . . . . . . 146
4.6 MSIBA WA PAMOJA . . . . . . . . . . . . . . 146
4.6.1 Takriri . . . . . . . . . . . . . . . 148
4.6.2 Sitiari . . . . . . . . . . . . . . . 148
4.6.3 Tashbihi . . . . . . . . . . . . . . 149
4.6.4 Chuku . . . . . . . . . . . . . . . . 150
4.6.5 Methali na Misemo . . . . . . . . . 151
4.6.6 Lugha ya Kishairi . . . . . . . . . 152
4.7 SIRI YA BWANYENYE . . . . . . . . . . . . . 153
4.7.1 Tashbihi . . . . . . . . . . . . . . 154
4.7.2 Taswira . . . . . . . . . . . . . . . 157
4.7.3 Chuku . . . . . . . . . . . . . . . . 157
4.7.4 Tashihisi . . . . . . . . . . . . . . 158
4.7.5 Kinyume . . . . . . . . . . . . . . . 158
4.7.6 Muundo wa Sentensi . . . . . . . . . 160
4.7.7 Ishara . . . . . . . . . . . . . . . 161
4.7.8 Nyimbo . . . . . . . . . . . . . . . 162
4.7.9 Nahau na Maneno ya Kiingereza . . . 164
4.8 Lugha Katika Hadithi Zote Nne Kwa Ufupi . . 165
4.9 KIMALIZIO . . . . . . . . . . . . . . . . . 167

**SURA YA TANO** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 170
PLOTI, USIMULIZI NA WAHUSIKA . . . . . . . . . 170
5.1 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . 170
5.2 PLOTI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 170
5.2.1 Sifa na Nafasi ya Ploti Katika Fasihi . . . . . . . . . . . . . . 172
5.2.2 PLOTI KATIKA HADITHI FUPI . . . . . 175
5.2.3 PLOTI YA SIRI YA BWANYENYE . . . . . 176
5.2.4 PLOTI YA MSIBA WA PAMOJA . . . . . . 178
5.2.5 PLOTI YA WASUBIRI KIFO . . . . . . . 181
5.2.6 PLOTI YA KICHEKO CHA USHINDI . . . . 184
5.2.7 Ploti Katika Hadithi Zote Nne . . . 187
5.3 USIMULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . 189
5.3.1 Mbinu za Usimulizi . . . . . . . . . 190
5.3.2 Usimulizi Maizi . . . . . . . . . . 190
5.3.3 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu . . . . . 192
5.3.4 Usimulizi wa Nafsi ya Kwanza . . . . 193
5.4 USIMULIZI KATIKA HADITHI FUPI . . . . . . . 195
5.4.1 Usimulizi wa Msiba wa Pamoja . . . . 195
5.4.2 Usimulizi wa Kicheko cha Ushindi . . 198
5.4.3 Usimulizi wa Wasubiri Kifo . . . . . 200
5.4.4 Usimulizi wa Siri ya Bwanyenye . . . 202
5.4.5 Usimulizi Katika Hadithi Zote kwa Ufupi . . . . . . . . . . . . . . . 204
5.5 WAHUSIKA . . . . . . . . . . . . . . . . . 204
5.5.1 DHANA NA DHIMA YA WAHUSIKA KATIKA FASIHI . . . . . . . . . . . . . . 205
5.5.2 Dhana ya Wahusika . . . . . . . . . 206
5.5.3 Dhima ya Wahusika . . . . . . . . . 207
5.5.4 UUMBAJI WA WAHUSIKA . . . . . . . . 208
5.5.4.1 Lugha na Fikra . . . . . . . 209
5.5.4.2 Wasifu (Umbo) . . . . . . . 210
5.5.4.3 Matendo . . . . . . . . . . 210
5.5.4.4 Uteuzi wa Majina . . . . . . 211

5.5.5 UWASILISHAJI WA WAHUSIKA . . . . . . 212
5.5.5.1 Uwasilishaji Dhahiri . . . . 212
5.5.5.2 Wahusika Kujifafanua . . . . 214
5.5.5.3 Mhusika Kujifafanua Mwenyewe 214
5.5.5.4 Mhusika Kufafanuliwa na Wahusika Wenzake . . . . . . 215
5.5.5.5 Uwasilishaji Katika Matendo . 215
5.5.6 AINA ZA WAHUSIKA . . . . . . . . . . 217
5.5.6.1 Wahusika Mviringo . . . . . . 217
5.5.6.2 Wahusika Bapa . . . . . . . . 218
5.6 WAHUSIKA KATIKA HADITHI FUPI . . . . . . . 219
5.6.1 WAHUSIKA WA SIRI YA BWANYENYE . . . 220
5.6.1.1 Ndugu Niyetu . . . . . . . . 220
5.6.1.2 Bi. Kessy . . . . . . . . . . 225
5.6.1.3 Salama . . . . . . . . 228
5.6.1.4 Wahusika Wengine . . . . . . 230
5.6.2 WAHUSIKA WA WASUBIRI KIFO . . . . . 231
5.6.2.1 Lugola . . . . . . . . . . . 231
5.6.2.2 Mgole . . . . . . . . . . . . 233
5.6.2.3 Wahusika Wengine . . . . . . 234
5.6.3 WAHUSIKA WA KICHEKO CHA USHINDI . . 235
5.6.3.1 Rajabu . . . . . . . . . . . 235
5.6.3.2 Subira . . . . . . . . . . . 236
5.6.3.3 Fatuma . . . . . . . . . . . 238
5.6.3.4 Bi. Khadija . . . . . . . . . 239
5.6.4 WAHUSIKA WA MSIBA WA PAMOJA . . . . 240
5.6.4.1 Kidawa . . . . . . . . . . . 240
5.6.4.2 Idi . . . . . . . . . . . . . 242
5.6.4.3 Dau . . . . . . . . . . . . . 243
5.6.4.4 Mahaja na Mama Tatu . . . . . 244
5.6.4.5 Mwajina . . . . . . . . . . . 245
5.6.4.6 Naomba . . . . . . . . . . . 245
5.7 VIPENGELE VINGINE VYA FANI . . . . . . . . 246
5.7.1 Ucheshi . . . . . . . . . . . . . . 246
5.7.2 Mzaha . . . . . . . . . . . . . . . 248
5.8 MUUMANO WA VIPENGELE VYA FANI KATIKA HADITHI FUPI . . . . . . . . . . . . . . . . 249
5.9 KIMALIZIO . . . . . . . . . . . . . . . . 255

**SURA YA SITA** . . . . . . . . . . . . . . . . . 258
HITIMISHO LA TASNIFU . . . . . . . . . . . . 258
6.1 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . 258
6.2 Muhtasari wa Kiini cha Tasnifu . . . . . . 258
6.3 Mahitimisho . . . . . . . . . . . . . . . 263
6.4 Mambo Muhimu Yaliyoibuka Kutokana na Utafiti Huu . . . . . . . . . . . . . . . . . 266
6.5 Mapendekezo . . . . . . . . . . . . . . . 267

MAREJELEO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 269

KIAMBATISHO 1 . . . . . . . . . . . . . . . . . . 287

KIAMBATISHO 2 . . . . . . . . . . . . . . . . . . 289